**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

Simu Na.255-26-2963341/2963342/2963346
Nukushi: 255-26-296334
Barua Pepe:ps@jamii.go.tz
Tovuti:www.jamii.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S.L.P 573,
**40478DODOMA.**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA WAJANE DUNIANI 2023

**Dodoma, 19 Juni, 2023**

**Ndugu Wanahabari; *Siku ya Wajane Duniani*** huadhimishwa kila mwaka tarehe 23 Juni. Siku hii iliasisiwa na **Bw**. **Lord Loomba** ambaye alianzisha ***Loomba Foundation*** mwaka 2005 baada ya Baba yake kufariki tarehe 23 Juni mwaka 1954. Umoja wa Mataifa ulipitisha siku hii kuwa ya Kimataifa kupitia Azimio **Na. A/RES/65/189** la tarehe 21 Desemba, 2010.

**Ndugu Wanahabari;** Kutokana na changamoto mbalimbali wanazopata Wajane, Nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa ziliazimia kuadhimisha siku hii tarehe 23 Juni kila mwaka kwa lengo la kuongeza uhamasishaji wa kupinga ukiukaji wa haki za binadamu kwa Wajane ambao wengi au baadhi huachwa katika umaskini, hunyimwa haki zao za mirathi kama ardhi, haki za kuwalea watoto na mali nyinginezo walizochuma kwa pamoja na mwenza wake kabla ya vifo kutokea.

Aidha, baadhi ya Wajane pia hujikuta wanafukuzwa nyumbani mwao, hutengwa na kunyanyaswa na ndugu wa mume pamoja na jamii na wengine hulazimishwa kuolewa na ndugu wa marehemu pasipo ridhaa yao. Aidha, wajane wengine hukosa utetezi mbele ya vyombo vya sheria pale wanapotafuta haki zao

**Ndugu Wanahabari;** maadhimisho ya Siku ya Wajane Duniani hutoa fursa kwa Wajane na Wadau kutafakari Mipango, Mikakati, Mafanikio na Changamoto wanazokumbana nazo wajane kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika kutatua.

Vilevile, Tanzania huadhimisha Siku ya Wajane kwa lengo la kukuza hamasa, mshikamano na uelewa ndani ya jamii ili kuacha ukiukaji wa haki za binadamu kwa wajane. **Hivyo, maadhimisho haya yanatoa fursa ya pamoja ya kutambua changamoto za Wajane na namna ya kukabiliana nazo.**

**Ndugu Wanahabari;** Takwimu Duniani zinaonesha kuwa Wajane ni takriban millioni **258** na kati ya hao, Wajane **115** millioni wanadhulumiwa, wanafanyiwa ukatili, wanakabiliwa na umaskini na kutengwa na jamii. Kwa Tanzania, idadi ya Wajane ni **1,396,262**. Takwimu hii ni kwa mujibu wa matokeo ya mwaka ***2022 ya Sensa ya Watu na makazi.***

**Ndugu Wanahabari;** Kaulimbiu ya Siku ya Wajane mwaka huu inasema ***"Wezesha Wajane kwa Teknolojia Bora: Kuwainua Kiuchumi".*** Kaulimbiu hii imetokana na ile ya kimataifa inayosema ***"Innovation and Technology for Gender Equality"*** ambayo inahimiza uwekezaji kwenye teknolojia rahisi na rafiki kwa lengo la kuwawezesha Wajane kuendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia.

Kaulimbiu hii inasisitiza kuwezesha jamii ikiwemo ya Wajane kutoa kipaumbele katika matumizi ya teknolojia rahisi na rafiki zikiwemo za kiganjani zitakazo wawezesha kupata suluhisho la matatizo yao kama vile elimu kuhusu Mirathi, Ardhi, Fursa za kiuchumi na Sheria mbalimbali.

**Ndugu Wanahabari;** Serikali inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** inawatambua na kuwajali Wajane ambapo, juhudi mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa kuhakikisha changamoto zinazowakabili zinatatuliwa ambapo, kwa ufupi Serikali imefanya yafuatayo;

1. Imeunda Wizara mahsusi ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambayo kwenye eneo la makundi maalum yanayoshughulikiwa ni pamoja na wajane.
2. Imeitambua Siku ya Wajane Duniani na kushirikiana na Wadau kushughulikia changamoto za Wajane.
3. Imeweka mifumo ya kulinda haki za Wajane kwa kuongeza Huduma za Msaada wa Sheria kutokana na kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria Na. 1 ya mwaka 2017.
4. Mwaka 2021 Serikali ilitoa msaada wa kisheria kwa Wajane ambapo Kesi 277 za Mirathi zilitolewa hukumu ya ushindi. Hii ni pamoja na uendeshaji wa mashauri na hukumu katika utetezi wa mali;

5. Imeanzisha Madawati ya Jinsia na Watoto 420 katika Vituo vya Jeshi la Polisi; Vituo 153 katika Jeshi la Magereza kwa lengo la kutokomeza ukatili wa Kijinsia kwa Wahanga wakiwemo Wajane;
6. Imeanzisha Kampeni ya ***“Maadili yetu Taifa letu – Kuwatunza na kuwalinda Wajane ni moja ya Maadili yetu”*** kwa ajili ya kuelimisha jamii kuachana na ukatili wa kijinsia kwa kushirikisha Wanaume;
7. Inahamasisha Wajane kujiunga kwenye vikundi na kuwezeshwa kwenye miradi mbalimbali ya ujasiriamali kupitia mikopo ya halmashauri ya 10%. Vilevile, ziko program mbalimbali za uwezeshaji wanawake kiuchumi wakiwemo na Wajane.
8. Wizara inaendelea kuratibu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, mikopo yenye thamani ya Shilingi Milioni 664.5 ilitolewa kwa Wanawake Wajasiriamali 104 wakiwemo Wanawake Wajane.
9. Serikali imewezesha kutungwa kwa Sheria ya Ardhi ya Kijiji Namba 5 (1999), Kifungu cha 20(1), ambacho kinatoa nafasi kwa Wanawake wakiwemo Wajane kumiliki Ardhi.
10. Inatekeleza Mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18 - 2021/22) wakiwemo Wajane.

**Ndugu Wanahabari;** Wizara inatoa Wito kwa Uongozi wa Mikoa yote kuimarisha ushirikiano na Wajane kupitia Vyama vyao ili kutambua mahitaji yao na kuchukua hatua.

**Ndugu Wanahabari;** mwisho, naomba kutumia fursa hii kuwasihi Wadau wote kuungana na Serikali katika kufichua ukiukwaji wa haki kwa Wajane ili waweze kupatiwa msaada wa kisheria pale inapohitajika.

**Ahsanteni.**

Gwajima

Dkt. Dorothy Gwajima (**Mb**).
**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM.**